# *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*

Asanteni sana. Mwaweza kuketi.

2 Hili ni tukio lisilo la kawaida kabisa kwangu usiku wa leo, kwa sababu nimetazamia tangu mvulana mdogo kuwa na wakati mmoja ambao ningeweza kuwahudumia watu wa Maine. Wakati nikiwa mvulana mdogo tu nilizoea kuja hapa kuwinda karibu na Ziwa la Moosehead, Dimbwi la Squaw, Shamba la Pittston, nyuma katika maeneo hayo huko. Nami ningekutana na watu wazuri sana, nilishangaa tu kama Maine haikuwa imejaa watu wa aina hiyo. Na nimekuwa katika jiji lenu la kupendeza hapa siku mbili, nami nimeona ndivyo ilivyo, watu waaminifu kweli.

3 Unajua wanasema, "Ukarimu wa kusini," vema, wao... Nadhani huu ndio mnaouita, "Ukarimu wa kaskazini." Maana hao ni watu wazuri hapa kama nilivyowahi kuwaona maishani mwangu, huku nikiuzunguka ulimwenguni mara tano.

4 Kwa hiyo bila shaka nina furaha kuwa hapa usiku wa leo katika ukumbi huu wa kupendeza na kuona kusanyiko hili zuri kwa jiji la aina hii lililo mbali sana na miji mikubwa. Na shauku yenu, na—na upendo wenu kwa Kristo kujitokeza namna hii kwenye usiku wa kwanza kwa mtu, labda, hajawahi kusikia juu yangu hapo awali maishani mwako. Kwa hivyo hilo ni zuri kabisa. Nathamini hilo.

5 Samahani, tuna usiku mmoja tu. Nadhani kama tungekuwa na siku nane au kumi hapa kwa uamsho wa kawaida, Bwana angefanya mambo makuu kati yetu, ambayo atafanya usiku wa leo; tutatarajia, tunatarajia hilo.

6 Sasa, hatuji kuwakilisha dhehebu lolote lile la kanisa. Sisi...Mimi, mimi mwenyewe nilitawazwa katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Ndipo basi sikuwahi kamwe... Sikuliacha tu kanisa, nilianza tu kusimama katika pengo kati ya madhehebu mbalimbali, na kwenye mikutano hii tu ya kuwaombea wagonjwa. Na ule ushawishi ambao Bwana amenipa, sitaki ku—kuutoa wote kwa dhehebu moja; ni kwa ajili ya Mwili mzima wa Bwana Yesu Kristo, bila kujali ni wa kanisa gani.

7 Basi nilikuwa nikiwachunga ng'ombe sana katika siku zangu huko magharibi, nami niliona wakati tungewapeleka hao ng'ombe hadi msituni, mbona, msimamizi angesimama pale akiwachunguza wale ng'ombe kwenye ua hami. Nyakati nyingi nimeketi pale huku mguu wangu umeingizwa kwenye pembe ya tandiko, nikitazama. Naye huyo msimamizi hakuzingatia sana

chapa iliyokuwa kwenye ng'ombe, ilikuwa ni—ilikuwa ni ukoo wa huyo ng'ombe. Damu iliyokuwa ndani ya ng'ombe, alikuwa na kitambulisho, na ilibidi awe ni Hereford ukoo safi la sivyo asingeweza kwenda msituni. Hilo lilikuwa ndilo jambo kuu.

8 Na ninafikiri hivyo ndivyo itakavyokuwa Siku ya Hukumu: Haitakuwa ni chapa gani hasa tunayovaa, zaidi sana ni ile Damu tuliyo chini yake. Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, itakuwa ndiyo alama kwa watoto Wake. Baadhi yetu tunaweza kusema, "Sisi ni Methodisti," au "Baptisti," au "Assemblies of God," au "Imani ya Kimitume," au chochote kile, lakini itakuwa ni wale wote walio chini ya Damu, naamini, watakaoingia katika Siku ile. Na kwa hivyo ninatarajia kuwa pamoja nanyi huko kwenye kusanyiko hilo kuu ambalo wanadamu wote wamelitazamia, kote katika nyakati.

9 Sasa, sisi huzungumza kuhusu uponyaji wa Kiungu hasa katika mkutano wangu. Lakini uponyaji wa Kiungu sio kile tunachojaribu kuzingatia. Huwezi kamwe kulifanya kubwa jambo dogo. Uponyaji wa Kiungu ni ka—karama tu ya kumwasilisha Kristo katika njia ya uponyaji wa Kiungu kuuvutia usikivu wa watu ili kuwafanya wajue ya kwamba Yesu anawapenda. Na uponyaji mkuu ambao tunafuata ni uponyaji wa nafsi ya mwanadamu, ya kwamba watu waliozaliwa mara ya pili wana Uzima wa Milele, wala hawataangamia kamwe, bali watafufuliwa tena katika siku ya mwisho. Halafu basi unajichagulia kanisa.

10 Tunatoka hapa tushuke kwenye mji mwingine mdogo chini yetu hapa, Bangor, naamini, Maine. Nasi tutakuwa huko mwishoni mwa juma hili na mwanzoni mwa juma lijalo, siku sita. Kitakuwa ndicho kipindi kirefu sana tumekuwa nacho katika . . . katika uamsho wa New England. Na kama wewe ni . . . unaishi karibu na hapo, tutakuwa tukitarajia kukuona, kwa hamu kuu. Na kutarajia, labda, katika mkutano huo, ambapo labda tutafahamiana zaidi. Siku moja, mbili usiku unajikuta ukisema, "Vema, nashangaa." Baada ya kitambo kidogo, kisha tunaondoka, "Kwaherini," nawe hupati kuwaona tena. Lakini tunapoweza kujumuisha siku chache usiku, mpaka unaweza kuona Mungu ni halisi, amethibitishwa kuwa halisi.

11 Sasa, ninaamini ya kwamba, mada ya uamsho huu ni, ya kwamba Yesu Kristo anabaki yeye yule, jana, leo, na hata milele. Sasa, tungependa kusoma Maandiko machache kwa muda mfupi tu.

12 Nami ninataka kuwaambia wale wanaofadhili hapa, kwa mchungaji, hakika tunawashukuru kwa ajili ya fursa hii, ndugu zangu wapendwa. Nami ninaomba kwamba Mungu wa Mbinguni atawabariki sana kwa wingi, na kuwapa shauku ya moyo wenu.

13 Sasa, kabla hatujafungua Neno Lake la thamani, mwanamume yeyote ambaye, au, mwanamke, mtoto, aliye na uwezo kimwili, anaweza kufungua kurasa, bali inahitaji Roho Mtakatifu kulifungua Neno moyoni mwetu, kwa maana limeandikwa na Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, "Hata watu wa kale, walipoongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Biblia." Hivyo basi, limevuviwa.

14 Hakuna binadamu aliye na haki ya kusema, "Tunayo tafsiri, hakuna mtu mwingine aliye nayo." Roho Mtakatifu anayo tafsiri. Basi hebu tumwombe usiku wa leo kama atatufasiria, tunaposoma na kuomba. Twaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda tu kwa maombi?

15 Sasa, hasa kwenu ninyi watu ambao hamjawahi kuwa mkutanoni hapo awali, ninawatakeni muwe waaminifu sana sasa, na kusema, "Mungu, niruhusu niweke kando kila chuki moyoni mwangu."

Ninyi mlio hapa ambao ni wagonjwa, semeni, "Mungu, unirehemu, hakika huu utakuwa usiku wangu wa uponyaji."

Acha mwenye dhambi aseme, "Mungu, unirehemu mimi mwenye dhambi," wakati tunapoomba.

16 Mungu Mtakatifu sana na mchaji sana, tunakuja katika Uwepo Wako, kwanza katika Jina la Bwana Yesu. Kwa maana tumefundishwa na Neno Lake takatifu lililobarikiwa, kwamba kama tukimwomba Baba lolote kwa Jina Lake, tutalipokea. Kwa hiyo basi, hatuna jina wala heshima ya kukutana Nawe. Nasi tunakuja kwa unyenyekevu, kwa uchaji katika Jina Lake tukufu na takatifu, tukijua kulingana na Neno Lake, ya kwamba Wewe utasikia, nasi tutakuwa na mazungumzo haya pamoja Nawe.

17 Sasa, mkutano huu umewekwa pamoja, Baba, Wewe umeangalia kila hatua, wala si kwa kusudi lingine, bali kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kwa msaada wa Kanisa Lake kuu, Mwili wa Mwanawe, usioonekana.

18 Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utawaponya wagonjwa wote walioko humu jengoni usiku wa leo; jalia kusiwe na mtu mnyonge atakayeondoka kwenye jengo hili pasipo kuponywa kikamilifu. Jalia mwenye dhambi, Bwana, asiyeamini, aaibike na kutahayari sana katika Uwepo wa Roho Mtakatifu mkuu, hata mwanamume au mwanamke huyo atasema, "Mungu unirehemu," na kuokolewa usiku huu.

19 Jalia, Bwana, kwamba wale ambao kidogo wananyauka, wanaanguka njiani, mikono hiyo dhaifu ambayo imekuwa ikining'inia chini, wale wanaoingia baridi na kutojali wanapokungojea kule Kuja, jalia wapate ujasiri mpya usiku wa leo, na wainuke katika nguvu za Bwana.

20 Mungu, jalia kwamba utatoa kitu, baraka katika ujirani huu, usiku wa leo, itakayoanzisha uamsho wa mtindo wa kale katika

kila nyumba, katika kila kanisa, na kila mahali nchini kote. Bwana, tunatambua kuwa hatuna muda mwingi sana uliosalia, kulingana na ka—kalenda ya wakati, kufanya kazi, kwa sababu jua linatua upesi na wakati wa mwisho umekaribia.

21 Kwa hiyo tusaidie kujiendeleza, usiku wa leo, kama watoto Wako wapendwa. Na ufanye kazi kupitia kwetu kwa Roho Mtakatifu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwanao mpendwa, Yesu. Amina.

22 Ningependa kuliendea Neno sasa, Andiko dogo tu ninalotumia kwenye, kwa kawaida, usiku wa kwanza, kutambulisha kwenu wito ambao Roho Mtakatifu amenipa.

23 Na, kwa uthabiti nikiwa mtu wa kimsingi ambaye anaamini Neno la Milele la Mungu: nikiamini kwamba kila kitu ambacho Mungu ameandika ni sehemu Yake Mwenyewe! Ninaamini Maandiko yanasema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Kwa hiyo basi, Neno hili ni sehemu ya Mungu. Na kama tutalikaribia namna hiyo: kulikaribia Neno Lake kana kwamba tulikuwa tukimkaribia Yeye!

Kwa maana hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Kama nisingeweza kulikubali neno lako, nisingekuamini kwa lolote; vivyo hivyo na wewe kwangu.

24 Na hivyo ndivyo nifanyavyo na Mungu. Kama Mungu alitoa ahadi, na kama Yeye ni Mwenyezi Mungu, hana budi kudumu na ahadi Yake apate kudumisha cheo Chake kama Mwenyezi Mungu. Hawezi kutoa ahadi, na kisha aighairi. Ninaweza kutoa ahadi na inilazimu kuighairi. Utatoa ahadi na ikubidi kuighairi, kwa sababu sisi ni wanadamu, nasi tuna—tuna kikomo. Lakini Yeye hana kikomo. Mungu hawezi kupata hekima zaidi, mwerevu zaidi; Yeye alikuwa mkamilifu kwanza kabisa. Basi Mungu anapotoa kauli, ni kamilifu.

25 Na kama Mungu atatoa kauli katika hali ya hatari, vile anavyoiendea hali hiyo ya hatari, kama hali iyo hiyo ya hatari ikitokea tena, hana budi kuiendea vile vile, sawasawa na alivyofanya mara ya kwanza, la sivyo alifanya makosa jinsi alivyoiendea mara ya kwanza. Unaona, kama Mungu aliwaponya wagonjwa kwanza kabisa kulipokuwa na hali ya hatari, wakati Musa hakuwa na tiba kwa wagonjwa, naye Mungu akainua nyoka ya shaba nyikani na kufanya upatanisho kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka kwa sababu kulikuwa na hali ya hatari; basi hali hiyo ya hatari ikifikia mahali tena ambapo hakuna tiba ya kutusaidia, Mungu hana budi kutenda vivyo hivyo kwetu, la sivyo alikosea alipomtendea Musa. Yeye ni Mungu; hawezi kubadilika. Kamwe hajui zaidi wala pungufu; Yeye ni mkamilifu milele.

26 Nami nataka kusoma sehemu ya Neno Lake inayopatikana katika Yohana Mtakatifu 12 na kifungu cha 20, na kisha Waebrania 13:8 kwa ajili ya somo:

> *Basi palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu . . . waliokwea kwenda* kuabudu . . . *kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao . . . basi* walimjia *Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwambia, wakisema,* Mabwana, *sisi tunataka kumwona Yesu.*

Na katika Waebrania 13:8, imeandikwa:

> *Yesu Kristo ni yeye yule jana . . . leo, na hata milele.*

27 Sasa, tunataka kuangalia jambo hili: Je, unaamini ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Je, waweza kuamini hivyo kwa sababu Biblia inasema hivyo? Kama unaweza kuamini, ningekutaka wewe, uinue tu mkono wako, kila mwaminio. Vema, basi . . . Asante. Kama Mungu amesema kwamba Yeye ni yule yule, basi hana budi kuwa ni yule yule, la sivyo Maandiko yamekosea. Na kama Maandiko yamekosea mahali pamoja, ningeogopa kuyaamini, kwa maana yanaweza kuwa yamekosea mahali pengine. Inabidi yote yawe kweli au yote ni ya uongo.

28 Kwa mfano kama sote tungelikuwa katika chumba hiki, usiku wa leo, tukifa kwa njaa, ndipo milionea fulani mashuhuri aje mlangoni na kusema, "Kesho saa tatu, nitawapa watu hamsini, humu ndani, dola elfu moja." Hakuna mtu angeweza kuwa na imani. Kama angesema, "Nitampa mtu mmoja, humu ndani, dola elfu moja, kesho." Hakuna mtu angeweza kuwa na imani. Unaweza kuwa ndiwe, na unaweza usiwe. Njia pekee ungeweza kuwa na imani, ni kusema, "Nitampa kila mmoja wenu dola elfu moja." Basi sote tunaweza kuwa na imani.

"Atakaye, na aje," yasema Maandiko. Ni juu ya yeyote atakaye; ni juu yako kama utakuja. Mwaliko umetolewa.

29 Sasa, tunataka kuona, Wayunani hawa waliokuja kuabudu, walikuwa na shauku kwamba walitaka kumwona Yesu. Nami naamini, ya kwamba, hiyo ndiyo shauku ya kila moyo wa kila mtu aliyepata kusikia Jina Lake: wanataka kuona huyo ni Nani. Najua ndiyo shauku ya moyo wangu. Nami nina hakika ndiyo shauku ya kila moyo ulio hapa: "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

30 Naye akachukuliwa . . . Wayunani hawa walipelekwa kwa Yesu na mhudumu mmoja jina lake Filipo, ambaye alienda akamchukua Andrea, nao wakampeleka kwa Yesu. Sasa, kama shauku yao ilikuwa ni kumwona, nao wakamwona, na shauku yetu ni kumwona, nayo Biblia ilisema ya kwamba Yeye hudumu yeye yule jana, leo, na hata milele, basi kwa nini hatuwezi kumwona?

31 Sasa, katika jiji langu, kulikuwa na mvulana mdogo, wakati fulani uliopita, ambaye alichangamka sana katika shule yake ya Jumapili, ndipo alipoenda nyumbani akamwambia mama yake, "Mama, kuna mtu yeyote anayeweza kumwona Mungu huyu mkuu ambaye wanatuambia habari zake?"

Akasema, "Muulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili."

Naye akamwuliza mwalimu, ama, alimwuliza, hasa, akamwuliza huyo mwalimu wa kike, naye akasema, "Mwulize mchungaji."

Nao wakamwuliza mchungaji, naye mchungaji akasema, "Hapana, mwanangu, hakuna anayeweza kumwona Mungu na kuishi."

32 Naam, maskini huyo jamaa, hilo halikuiridhisha shauku yake. Kwa hiyo alikuwa akivua samaki huko juu mtoni pamoja na mvuvi mzee, kule chini, jina lake Wiseheart, alikuwa shemasi kanisani mwetu. Naye, siku moja, akishuka mtoni, kukatokea tufani; kilikuwa ni kiangazi kilichojaa mavumbi, na maji yalikuwa yamefagilia mbali majani yote; nalo jua lilikuwa linatua magharibi, wakati huyo mvuvi mzee, huyo mvulana mdogo, waliposhuka chini baada ya kutega nyavu. Ndipo ukaja upinde wa mvua. Ndipo huyo mvuvi mzee alipotazama upinde huo wa mvua, jamaa huyo mdogo aliona kwamba machozi yalianza kutiririka chini ya mashavu yake yenye ndevu.

33 Na machozi yale maangavu yakitiririka kwenye ndevu zake nyeupe, kidogo yakachochea hisia za maskini mvulana huyo. Basi akakimbia kutoka shetri ya mashua hadi katikati, akaanguka kwenye mapaja ya huyo mvuvi mzee, akasema, "Bwana, nitakuuliza jambo ambalo, inaonekana, hakuna mtu anayeweza kunijibu."

Naye akasema, "Ni nini, mwanangu?"

Akasema, "Mungu ni mkuu sana, Mungu aliyeumba upinde ule wa mvua." Kasema, "Je, kuna yeyote anayeweza kumwona Mungu?"

34 Ndipo huyo mvuvi mzee, huku amelemewa na shauku ya huyo mtoto, alimshika mikononi mwake, akasema, "Mungu aubariki maskini moyo wako, kipenzi, yote ambayo nimeona kwa miaka arobaini imekuwa ni Mungu." Njia ya kumwona Mungu ni kumwingiza Mungu ndani, ndipo Yeye anatazama kupitia kwa macho yako. Ndipo unamjua, unaweza kuelewa, atajifunua Mwenyewe.

35 Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo, nao ulimwengu, hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Mtu yeyote asomaye Maandiko anajua hiyo ni kweli. Basi ni ahadi ya Yesu, kwa Neno Lake Mwenyewe: kwamba ku—kungekuwako na watu ambao wangemwona mpaka atakapokuja

tena mwishoni mwa ulimwengu. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi . . . " (kiwakilishi nafsi) " . . . nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Sasa je, Maandiko hayo ni kweli? Au alikuwa akiwatania tu wanafunzi? Kama alikuwa akiwatania, na kuwachezea, na kupayuka, basi Yeye hakuwa Mwana wa Mungu. Hiyo ama ni kweli, au si kweli.

36 Na sasa, mnasema, "Vema, Ndugu Branham, ninaamini ya kwamba Mungu anaishi katika maua." Nami pia. Lakini Wayunani hawa walitaka kumwona Yesu, walitaka kumwona. Sasa, Yeye alisema, katika Maandiko, katika Maandiko, ya kwamba, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Sasa, ili kuhalalisha kauli hii, basi, ingetubidi kurudi katika Maandiko na kuona kile Yesu alichokuwa jana, tukitaka kujua atakachokuwa leo.

37 Sasa, nataka kuwaulizeni, wasikilizaji, usiku wa leo, hilo si lingekuwa jambo zuri mbele ya Wamethodisti, Wabaptisti, Wakatoliki, na Waprotestanti na *kadhalika*? Kila mmoja akisema, "Kanisa langu linaamini *hivi*." "Kanisa langu linaamini *hivi*." Ambalo ni sawa kabisa, lakini kama kweli unataka kuona kile alichokuwa jana, ili ujue kile Yeye alicho leo, ni kurudi katika Maandiko na kuona kile Yeye alichokuwa jana. Ndipo hatuna neno la kanisa, tuna Neno la Mungu Mwenyewe kulihusu.

38 Sasa, kile alichokuwa jana, hana budi kubaki Yeye yule leo, la sivyo Yeye si yeye yule jana na leo. Sasa, katika ahadi Yake Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya," Najua ya King James, hapa, inasema, "kubwa zaidi," lakini ukipata tafsiri sahihi, ya asili juu yake, inasema "nyingi zaidi." Hakuna mtu angeweza kufanya kubwa zaidi; Yeye alikomesha maumbile, akawafufua wafu, akawaponya wagonjwa, loo, alifanya kila kitu. Huwezi kufanya kubwa zaidi, lakini Mungu, Roho Mtakatifu angekuwa katika Kanisa la ulimwengu mzima, kote ulimwenguni kwa wakati mmoja. Ni kama tu maji yote ya baharini. Hayo ndiyo . . .

39 Mungu alimpa Yesu Roho bila kipimo. Ndani Yake mlikaa Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Biblia ilisema kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Lakini anapotoa Roho Wake kwetu sisi wana wenye mamlaka, anatupa ndoo nzima kutoka katika bahari hiyo. Alikuwa na Utimilifu wote wa Uungu; tunayo tu sehemu Yake, kama kipawa, cha Roho Mtakatifu.

40 Lakini kama nilichota ndoo moja iliyojaa kutoka baharini, au hata kijiko kimoja cha maji, kutoka baharini, kemikali zile zile zilizo kwenye hiyo bahari nzima, zingekuwa kwenye kijiko hicho. Itakuwa kidogo tu katika kipimo, si pungufu katika ubora

wake. Kwa hiyo Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa ndani ya Kristo yuko ndani ya Kanisa Lake.

41 Sasa, sikilizeni, ili kuimarisha hilo kwenu. Alisema, "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi." Sasa, m—mzabibu hauzai tunda. Mzabibu hulisafisha tu tawi nalo tawi linazaa tunda. Kwa hiyo, njia pekee Yesu angeweza kunena usiku wa leo, ingekuwa kupitia midomo yangu au midomo yako, mikono yangu au mkono wako, maisha yangu au maisha yako. "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Yeye hazai tunda tena, Yeye hulitakasa tu Kanisa Lake nalo linazaa tunda.

42 Sasa, lingezaa tunda la aina gani? Kama Uhai uliokuwa ndani Yake uko ndani ya Kanisa Lake, litazaa Maisha yale yale aliyozaa alipokuwa hapa. Mnaelewa?

43 Angalia, kama ulienda kwenye mzabibu, ungetarajia kupata zabibu. Na huko kusini, sijui kama mnayo hapa, tuna maboga kule chini. Na ukienda kwenye tawi la mboga, unatarajia kupata maboga, ikiwa ni tawi zuri, lenye rutuba. Tikiti maji, utapata tikiti maji kutoka kwa mmea wa tikiti maji.

44 Na kama tukija kwenye Mzabibu, Kristo, kanisa Lake, tunapata nini? Mzozo, hamaki, mabishano juu ya theolojia, chuki, kijicho, ugomvi; nasi tunayaita hayo matendo ya Mungu. Maandiko yanasema sivyo. "Hivyo, watu wote watatambua wakati ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Upendo wa Mungu katika Kanisa Lake, ukimfanya kila mshiriki kuwa sehemu Yake, ndipo juu ya mwamba huo na msingi huo, Yeye hulijenga Kanisa Lake.

45 Angalieni, sasa nisije nikachukua muda wenu mwingi sana, saa nyingi zingeweza kutumika kwa hilo, tukionyesha yale aliyoahidi, lakini sasa, somo ni: Je, Yeye ni yeye yule leo ambaye alikuwa wakati huo? Je, Yeye ni yeye yule kwa kila njia, ila mwili wa kawaida? Sasa, mwili Wake utakapokuja, basi tutaenda nyumbani pamoja Naye.

46 Kwa maana mwili Wake umeinuliwa na kuketi juu ya kiti cha enzi cha Mungu, usiku wa leo, kufanya uombezi tunapoungama. Yeye ni Kuhani, Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Waebrania 3:1. Basi ameketi pale kama Kuhani Mkuu. Nami naomba niseme hivi: hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na wanadamu, ila Yesu Kristo; Maandiko yanasema hivyo. Na Yeye Ndiye pekee anayesimama kati ya Mungu na wanadamu kufanya uombezi. Nayo Maandiko yanasema kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

47 Sasa, hebu turudi nyuma tuone Yeye alikuwa ni nini. Nilisoma kutoka katika Yohana Mtakatifu 12. Sasa, kwenu ninyi watu wapendwa hapa kutoka ma—maeneo na mji jirani, mkifika nyumbani usiku wa leo, ama asubuhi, katika utulivu wa mchana, ninyi wanawake, mumeo anapokuwa kazini, ama wewe, bwana, kabla tu hujalala kitandani usiku wa leo, ama kesho usiku, saa

yako ya adhuhuri, kama umebeba Biblia yako, fungua Yohana Mtakatifu 1, tuone Yeye alikuwa nini jana. Sasa, Maandiko yo—yoyote yatamtangaza, lakini tunasoma katika Yohana Mtakatifu 1.

48 Baada ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu, Mungu alikuja na kudhihirishwa, siku arobaini nyikani, akatoka, na akaanza huduma Yake.

49 Sasa, ninataka kuwaulizeni swali, nami nataka mnijibu kwa kuinua mkono wako. Kama tunaweza kujua kile alichokuwa jana, Naye atakuja hapa usiku wa leo miongoni mwenu enyi watu na kujitangaza Mwenyewe leo kama alivyokuwa jana, ni wangapi wenu watakaompokea? Hebu tuone mkono wako, ukiinuliwa juu hewani sasa, kila mwaminio. Asante. Hebu tuangalie kile alichokuwa.

50 Sasa, kwanza kabisa, sababu ya jambo hili kutokea leo, ni kwa sababu huu ndio mwisho wa wakati wa kanisa la Mataifa. Sasa, wasomi wowote wanajua jambo hilo; kwamba tuko mwishoni. Yesu alipokuwa hapa katika mwili wa nyama, hakwenda kwa Mataifa. Naye akawakataza wanafunzi Wake kuwaendea Mataifa. Akasema, "Sikutumwa kwao; afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa Israeli. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, 'Ufalme umekaribia,' na kadhalika." Na Yeye kamwe hakuwaendea Mataifa kwa sababu kulikuwa na nafasi ya miaka elfu mbili kuliita kanisa litoke, kupitia kwa mataifa yote.

51 Lakini katika Yohana Mtakatifu 1, tunaona ya kwamba kulikuwa na mtu, aliyeokolewa, na upesi, akaenda akamwita ndugu yake. Sasa, hiyo ni ishara nzuri kwamba aliokolewa: alienda na kumpata ndugu yake.

52 Basi alipomleta ndugu yake Kwake, Yesu, yeye alikuwa mvuvi, nayo Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe. Ndipo alipokuja Mbele za Bwana Yesu, Yesu akamwambia, "Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona." Mnafikiri mvuvi huyo asiye na elimu wala maarifa alifikiria nini, wakati Mtu Ambaye hajawahi kumuona maishani mwake, ama wala hakuwahi kumwona Mtu huyu, alipokuja Uweponi Mwake, akamwambia yeye alikuwa ni nani na baba yake alikuwa nani? Je, kuna mtu aliyewahi kusoma jambo hilo katika Maandiko? Hakika: Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, yapata kifungu cha 8.

53 Ndipo mtu huyu akamtazama na akawa mtumishi wa Bwana Yesu; jina lake aliitwa Kefa na Bwana Yesu, baadaye. Basi huyo alikuwa Mtakatifu Petro, yule mtu ambaye hakuweza kuandika jina lake mwenyewe, mtu aliyeitwa asiye na elimu wala maarifa, alikuwa amekabidhiwa funguo za Ufalme mkononi mwake.

54 Sasa, mnaona kile tumefanya nalo? Tumejaribu kuwaleta watu kwa Kristo kwa kuwaelimisha. Hata afadhali uyasahau. Hakuna mpango mwingine utakaofanya hivyo ila mpango wa mtindo wa kale, kuzaliwa upya. Kuzaliwa mara ya pili ndiyo njia pekee itakayoweza kuwa. Tumejaribu ku—kuwaelimisha; tumejaribu kuunda chama, na kadhalika, kuwaleta watu kwenye udugu. Nao unawatenganisha mbali zaidi na Mungu. Nasi tunakuwa na ubaguzi, na kujenga kuta za kimadhehebu, na kujitenga na hao ndugu wengine.

55 Lakini kisa kizuri kweli, cha ubatizo wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu moyoni mwako, kitakufanya usahau kiburi chako. Kitamfanya aliyevalia suti rasmi kumkumbatia aliyevaa ovaroli na kumwita, "Ndugu." Kitafanya aliyevaa vazi la hariri kumkumbatia aliye na la kaniki, aseme, "Dada." Kinafanya kitu ndani yako ambacho kinaenda mbali kuliko dhana ya kiakili; ni kuzaliwa kwa roho inayoishi ndani ya moyo wa mwanadamu.

56 Sasa, mara tu alipomwambia Simoni jambo hilo, akawa mtumishi Wake. Mara moja, basi, Filipo alifurahi sana naye akasema alikuwa na rafiki mwingine, ndipo akazunguka mlima, maili kumi na tano, kumtafuta rafiki yake Nathanaeli. Hebu tumfuate kwa dakika chache tu. Naye anamwendea na labda Bibi Nathanaeli alikuwa nyumbani, naye anasema, "Nathanaeli yuko wapi?"

"Loo, alitoka kwenda bustanini muda mfupi uliopita."

57 Huyo akaenda kwenye shamba la matunda, na hapo akamkuta Nathanaeli huko nje chini ya mti, kama vile mtu yeyote mzuri mwaminifu angekuwa, akiomba. Kama muungwana Mkristo, bila shaka hangemkatisha alipokuwa akiomba. Akisha kumaliza, ninaweza tu kumwona Nathanaeli akisimama na kusema, "Kweli, ikiwa huyu si Filipo."

Sasa mwangalieni; ana ujumbe. Bila kupokea utangulizi wake wala chochote, alisema, "Njoo, uone Yeye tuliyempata."

58 Sijui nini kingetukia kama kundi hili dogo la watu, hapa katika jengo hili usiku wa leo, lingekuwa na shauku hivyo juu ya Yesu. Sijui nini kingetukia kama mojawapo ya makanisa haya madogo hapa yangepata shauku juu ya Yesu, kwamba yote yaliyoko moyoni mwako, wako—wako wa kwanza ni wa kwanza, na huyo ni Mungu. Jambo la kwanza ni Yesu. "Njoo, umwone Yeye tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

59 Loo, sasa, unajua, jamaa huyu hapa, Nathanaeli, alikuwa mwothodoksi, mnyoofu sana, jamaa mzuri. Nami naweza kumsikia akimwambia Filipo, "Sasa, ngoja kidogo, Filipo. Hapana shaka umeingia wazimu. Je, unataka kuniambia kwamba Mwana wa Mungu angetoka Nazareti, hilo kundi dogo la watu huko chini ambalo ni katili? Kama Mwana wa Mungu, Masihi, angalikuwa hapa, Yeye angekuja hekaluni. Angekuja kwa . . . angekuja Yerusalemu wala si Nazareti."

Ninasema hivi kwa upendo na heshima, lakini hivyo ndivyo wanavyofikiria siku hizi, hawawezi kuamini.

Loo, wewe Mkatoliki ungesema, "Angekuja kwenye Jiji la Vatikani; angemjulisha papa."

Na ninyi Wapresbiteri mngesema, "Loo, angemjulisha askofu"; na kadhalika, sisi sote.

60 Lakini Mungu hufanya mambo kwa njia Yake Mwenyewe. Na sikuzote ni kinyume na jinsi makasisi walivyowazia, sikuzote. Ninyi wanahistoria mnajua hilo. Kamwe hakuna wakati wowote makasisi wamelipata.

61 Kwenu ninyi Wakatoliki . . . Kwenu ninyi Waprotestanti kwanza: Vipi kuhusu Eliya? Hawakuamini alikwenda Nyumbani kwa gari la farasi. Waliwatuma watoto wao wadogo nyuma ya Elisha, wakisema, "Ewe mwenye upara, kwa nini hukupaa juu?" Ndipo huyo nabii akawalaani watoto hao. Nayo laana ikawajilia, ndipo dubu wawili wa kike wakaua watoto wadogo arobaini na wawili.

62 Vipi kuhusu Musa? Yesu alipokuwa hapa, alisema, wanafunzi walimwambia, kasema, "Kwa nini Waandishi wanasema, hao wahudumu, kwa nini wanasema ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?"

Akasema, "Tayari amekuja, wala hamkumtambua." Nao walijua alinena juu ya Yohana Mbatizaji.

63 Sasa, kwako Mkatoliki. Vipi kuhusu Mtakatifu Patrick? Je, kanisa lilimtambua? Walidhani alikuwa ni mchawi. Lakini akisha kufa, na ujumbe umetolewa, ndipo kanisa likampokea. Vipi kuhusu Mtakatifu Francis wa Assisi? mhubiri wa kutembea na Biblia chini ya mkono wake, ambaye alilipinga kanisa Katoliki. Alipoenda kuhubiri huko chini pembeni siku hiyo, wakati wale ndege wadogo walipokuwa wakipiga kelele, yeye alisema, "Akina dada, simameni kimya; tulieni ninapohubiri." Nao wakamtii. Naye akiisha kufa, sasa ametangazwa rasmi kama mtakatifu katika kanisa lenu.

64 Vipi kuhusu Joan wa Arc? Msichana yeyote wa shule angejua habari zake, msichana mdogo ambaye aliona maono, na Malaika, na kupata mafunuo. Nalo kanisa lenu, kanisa Katoliki, likamchoma moto kwenye nguzo, akilia apate rehema, wakimwita kitu kile kile walichomwita Yesu, Beelzebuli, mchawi. Joan wa Arc alichomwa moto kama mchawi kwenye nguzo na kanisa Katoliki la Kirumi . . . ? . . .

65 Ndipo yapata miaka mia moja baadaye waligundua kwamba yeye hakuwa mchawi; alikuwa mtakatifu. Lakini Mungu akatuma ujumbe Wake, vivyo hivyo tu. Nao wakakosa kuuona. Hawakujua Mwana wa Mungu alikuwa ni Nani mpaka alipokuwa amekufa, kuzikwa, na kufufuka tena. Mungu ni mwenye enzi; Yeye hufanya kazi Zake. Na ninii Lake . . . Kanisa

lazima liamke, hapa katika siku hizi za mwisho. Ni jambo la kusikitisha sana.

66 Majuma machache yaliyopita katika jiji langu la Louisville, kulikuwa na mama mmoja aliyekuwa akizunguka-zunguka, akiwa na mtoto mchanga, katika duka la mali rahisi. Naye alikuwa akimwonyesha vitu, akisema, "Angalia, mpendwa." Naye huyo jamaa mdogo akakodoa macho. Ndipo akamwonyesha kitu, "Sasa, tazama, mpenzi." Naye huyo jamaa mdogo aliendelea kukodoa macho. Moja kwa moja akaenda kwenye kaunta iliyokuwa na kipambo kidogo kilichotatarika, naye akakitikisa mbele zake. Naye huyo jamaa mdogo akakodoa tu macho yake moja kwa moja angani. Ndipo akaanguka kwenye kaunta amechoka na kulia.

67 Basi baadhi ya watu wakamwendea kuona kuna nini. Akasema, "Si muda mrefu uliopita alianza tu kukodoa macho, akitazama mbele moja kwa moja." Kasema, "Yeye ni mwanadamu mdogo, na anapaswa kutambua vitu vinavyohusu maisha haya ya mwanadamu. Daktari aliniambia, muda mfupi uliopita, alikuwa amepata nafuu, lakini," kasema, "hajapona."

68 Nami sijui kama hivyo sivyo tu kanisa lilivyo siku hizi. Mungu anatikisa kila aina ya karama mbele ya kanisa, nalo linakodoa tu macho na kutazama, kasema, "Vema, nadhani hiyo ni sawa kabisa; kama ingalikuwa katika dhehebu langu, huenda tungeliweza kuikubali."

69 Hivi hamwoni? Kanisa linakaa limepooza kiroho, badala ya kiakili. Kumekuwako na akina Billy Graham, kumekuwa na Oral Roberts, kumekuwako na watu mashuhuri, akina Jack Shuler, na *wengineo*, katika miaka michache iliyopita, ambao wamelichambua taifa hili. Na bado wananinii tu, kanisa linakaa tu: "Naam, mimi ni *hili*." Au, "Katika kanisa langu . . . " Mnapata mawazo hayo.

70 Naye Nathanaeli alikuwa na wazo lile lile. Alisema, "Sasa ngoja kidogo, kama kuna kitu chochote kizuri kinachoweza kutoka Nazareti, kisingekuwa ni Mwana wa Mungu, Huyo angekuja kwa kuhani mkuu."

71 Nami nafikiri Filipo alimpa jibu zuri zaidi ambalo mtu yeyote angeweza kumpa, alisema, "Njoo uone." Sasa hilo ni la busara, lenye mantiki, ni sahihi, "Njoo ujionee mwenyewe; usikae nyumbani. Njoo ujionee mwenyewe. Njoo uone."

Nami nitakwambia nini . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . na zaidi ya hayo, Yeye alimwambia baba yake alikuwa nani na jina lake lilikuwa nani."

"Loo, sasa hebu kidogo," Nathanaeli angemwambia Filipo, "Filipo, naamini uliingia wazimu."

"Wewe njoo ujionee mwenyewe."

72 Wakaingia katika umati wa watu pale Yesu alipokuwa. Wao. . .labda walikuwa huko nje kwenye—kwenye kusanyiko, ama labda walikuwa kwenye mstari wa maombi. Yesu alipomwona kwa mara ya kwanza, alisema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

73 Sasa, kumbukeni, mwanzoni mwa huduma Yake: Huyu hapa akijitambulisha Mwenyewe kwa kizazi cha Kiyahudi namna hii. "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

"Vema sasa," ungesema, "jinsi alivyokuwa amevalia . . . "

La, angalikuwa Mwarabu, angalikuwa Myunani, karibu taifa lolote; watu wote wa mashariki huvalia vile vile.

Kasema, "Tazama Mwisraeli . . . " Alijuaje alikuwa Mwisraeli? " . . . ambaye hamna hila ndani yake!"

74 Naye aliposema hivyo, lilimshangaza sana, akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe? Sijawahi kukuona Wewe, Nawe hujawahi kuniona. Ulinijua lini Wewe?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Ni wangapi wanaojua Maandiko yanasema hivyo? Huyo alikuwa ni Yesu jana; hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Myahudi.

75 Sasa, loo, kulikuwa na wale waliosimama karibu, ambao walikuwa ni wa makanisa makubwa mashuhuri, yale ya kiothodoksi; unajua waliyosema? Moyoni mwao walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni Beelzebuli. Huyasoma mawazo yao." Walisema hivyo mioyoni mwao, naye Yesu akayatambua mawazo yao.

76 Naye akasema . . . Sikilizeni, aliyosema Yeye: "Amin, nawaambia, mkisema hayo dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Ni wangapi wanaojua Maandiko yanasema hivyo? Basi tunasimama wapi usiku wa leo kama Yeye akijitangaza Mwenyewe kwa Roho Mtakatifu ya kwamba Yeye ni yeye yule tu?

77 Siku chache baadaye tunamwona katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4. Kabla tu ya kufunga. Nasi tunamwona katika mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu. Sasa Yeye hakuwaendea Mataifa. Hakufanya ishara hiyo hata mara moja kwa Mataifa, kwa Wayahudi tu. Lakini Huyu hapa, mbele ya Wasamaria. Naye akawatuma wanafunzi Wake, kwa sababu alikuwa amechoka, Naye akaketi katika mandhari ndogo, kitu kama *hiki, hapa*, ambapo kuna ninii . . . Ikiwa umewahi kuwa huko, kile kisima bado kiko, nje tu ya lango la Samaria. Yakobo alikichimba.

78 Na ni yapata wakati wa adhuhuri, nao wanafunzi wakaenda mjini kununua chakula. Basi wakiisha kuondoka, Yesu

akipumzika, kwa maana Yeye alifanya mahubiri, na uponyaji wa wagonjwa, na kadhalika, alikuwa amechoka na kudhoofika. Naye Baba, bila shaka, alikuwa amemwambia aende kule. Kwa sababu katika Yohana Mtakatifu 5:19, aliulizwa juu ya uponyaji wa mtu fulani, Naye akasema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda." Ni wangapi wamewahi kusoma hilo? Yohana Mtakatifu 5.

79 Basi Yesu hakufanya muujiza hata mmoja hadi Mungu alipomwonyesha kwa maono jambo la kufanya kwanza. Hilo hapo, Yohana Mtakatifu 5:19, "Sitendi neno Mwenyewe, ila lile nimwonalo Baba analitenda. Baba anatenda kazi nami natenda kazi vile vile." Hivyo ndivyo alivyosema.

80 Sasa, Huyu hapa, Baba alikuwa amemtuma huko juu Samaria, nao—nao wanafunzi walikuwa wamekwenda mjini. Basi hebu tuwazie kuwa alikuwa msichana mrembo. Anatoka, ingawa alikuwa na sifa mbaya, akaja kuteka maji. Ndipo alipoanza kushusha mtungi . . .

81 Ikiwa umewahi kuwa huko mashariki, wanaweza kuibeba vichwani mwao na nyongani mwao. Nao wanawake wote wanaenda kule, nao wana winchi; nao wanaizungushia kulabu hii ndogo, kisha wanaushusha na kuchota mtungi uliojaa maji, na kuweka mmoja juu ya kichwa chao, na mmoja kwenye kila nyonga. Na kutembea moja kwa moja, wakiongea, kama tu wanawake wanavyoweza, na kamwe wasimwage hata tone la maji, mtungi huo mkubwa ambao ni wa galoni mbili au tatu umewekwa kichwani mwao, na mmoja kwenye kila nyonga. Nao wanatembea tu moja kwa moja, wakiongea.

82 Basi mwanamke huyu akaja kuteka maji yake, labda, kama mnajua: alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, kwa hiyo hangeweza kuja kule wakati wengine wote, wanawake wakiwa pale. Hawakuchangamana kama wafanyavyo siku hizi.

83 Ndipo alipokuja kuteka maji, alitazama pale, na huyo hapo Myahudi ameketi, Mtu aliyekuwa na umri wa miaka thelathini na miwili tu, bali alionekana kana kwamba alikuwa na hamsini. Yohana Mtakatifu 6, aliposema, mle ndani walisema, "Unasema ulikuwa mkuu kuliko—kuliko Ibrahimu? Nawe ni mtu ambaye hujafikisha miaka hamsini bado? Tunajua sasa una pepo."

84 Naye akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Na huyo MIMI NIKO alikuwa ni ile Nguzo ya Moto katika kichaka kilichowaka moto (Mnajua hilo?), yule Malaika wa Agano. Naye alipokuwa hapa duniani, alisema, "Nalitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu." Hiyo ni kweli? Basi ile Nguzo ya Moto, yule Malaika wa Agano (ambapo Musa aliiacha Misri, akihesabu kushutumiwa Kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri), basi wakati alipofanyika mwili na kukaa katika mwili

hapa, Yeye alisema, "Nalitoka kwa Mungu na ninaenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli?

85 Na baada ya kufa Kwake, kuzikwa na kufufuka, Paulo alikuwa njiani kwenda zake Dameski kuwakamata wale watu waliokuwa wakipiga kelele nyingi sana. Ndipo Kitu fulani kikamwangusha chini: Nguzo ya Moto ikisimama pale, ilimpofusha. Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unanitesa Mimi?"

Akasema, "U nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Akarudi kwa Baba tena: Nguzo ya Moto. Hayo ni Maandiko.

86 Baadaye akaingia gerezani, walipokuwa wakiomba katika nyumba ya Yohana Marko, akafungua milango mbele ya mtume Petro na kumweka huru.

87 Na samahani hili kama linaonekana kama ni la kibinafsi. Kwenye picha hii usiku wa leo, mnaona ninii . . . si yangu, bali mnaona Nguzo ile ile ya Moto, ambayo George J. Lacy, mkuu wa FBI alisema hivyo: Ni Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopigwa picha kilichopata kuthibitishwa; kinaning'inia huko Washington, DC katika Ukumbi wa Sanaa za Kidini, huku jina la George J. Lacy limeitia sahihi; Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha. Ujerumani wanayo sasa, walipoipiga mwaka jana.

88 Kama Ndiyo, itafanya mambo yale yale ambayo ilifanya huko nyuma, kwa maana ni Mzabibu, na kama umeunganishwa katika matawi, utazaa nguvu zile zile, na Uwepo ule ule, na kazi zile zile. Hauna budi, kwa kuwa Yeye ni yeye yule.

89 Sasa, angalia kazi Zake uone kama ni Yeye au siye. Ihukumu kwa matunda inayozaa. Kama ni Roho yeye yule, basi atafanya jambo lile lile. "Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya."

Naye huyu hapa ameketi kisimani, naye mwanamke huyu alikuwa amesimama pale, Naye akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

Naye mwanamke akasema, "Tuna ubaguzi hapa. Si desturi kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho. Mimi ni mwanamke Msamaria."

Alisema, "Lakini mwanamke, kama ungejua ni Nani uliyekuwa ukiongea naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

90 Naye akasema, "Je, unasema kwamba kisima ni kirefu, Nawe huna kitu cha kuchotea, na ati Wewe ni mkuu kuliko baba yetu Yakobo aliyechimba kisima hiki, nao ng'ombe wake wakanywa?" na kadhalika.

Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Na mara alipopata shida yake ilipokuwa, alisema, "Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa."

Akasema, "Bwana, sina mume."

Akasema, "Hiyo ni kweli; unao. . .umekuwa na watano; na unayeishi naye si wako."

91 Sasa, alisema nini? "Wewe ni—wewe ni Beelzebuli"? "Una telepathia ya kiakili"? "Wewe ni mpiga ramli"? La, alijua zaidi kuhusu Injili kuliko nusu ya wahubiri huku Marekani, akiwa ni kahaba. Alijua mengi juu yake kuliko makasisi wenye elimu na marabi wa siku zake. Angalieni yale mwanamke huyu kahaba aliyofanya. Alimtazama moja kwa moja usoni, na akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, atafanya mambo haya." Je, hiyo ndiyo ishara ya Masihi? "Ajapo Masihi, tunajua, sisi Wasamaria, tunajua hii itakuwa ishara ya—ya Masihi. Atakapokuja, atafanya mambo haya. Lakini u Nani Wewe?"

Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye".

Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, haina budi kuwa vivyo hivyo leo, kama Yeye anadumu yeye yule, akijitangaza Mwenyewe.

Kuna Myahudi na Msamaria pia. Alijitangaza Mwenyewe.

Alifanya nini? Alikimbia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu, aliniambia mambo ambayo nimefanya: haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?"

92 Je, sisi Wakristo tungewazia nini kuhusu hilo usiku wa leo kama angefanya hivyo? Nashangaa tu. Huenda atafufuka Siku ya Hukumu na kuwahukumu wanazuoni wengi, na wahubiri, na makuhani siku hizi. Huyo mwanamke aliitambua.

Naye akasema, "Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyofanya: haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?"

Nao hao watu wakatoka, nao walipomsikia walishawishika ya kwamba alikuwa ndiye Masihi.

93 Sasa, angalieni, Yeye alifanya hiyo, hiyo ishara kwa Wayahudi, kuwathibitishia Wayahudi, kuwapata Wateule; na kutiwa muhuri kwa maangamizi, kuhani, na rabi, na asiyeamini. Filipo, wengine wote walimwamini.

Na ndipo alipojitambulisha kwa Msamaria, Yeye alifanya jambo lile lile.

94 Lakini hata wakati mmoja Yeye hakuwahi kufanya jambo hilo mbele ya Mmataifa, na kukataza lisitendwe. Kwa nini? Miaka elfu mbili imekuja sasa kwa ajili ya Mataifa kupata mafunzo na mafundisho.

95 Lakini mwishoni mwa kipindi cha wakati wa Kiyahudi, kabla hawajakutana na machafuko, kama Yeye alijitangaza Mwenyewe hivyo kwa Wayahudi kuthibitisha Yeye alikuwa ni Masihi, Naye alitenda hivyo kuthibitisha jambo hilo, Yeye hana budi kutenda jambo lile lile wakati wa kumalizia kwa Mataifa

la sivyo si yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaelewa? Inueni mikono yenu ikiwa mnaelewa. Mnaelewa hiyo ni kweli. Inambidi kufanya hivyo.

96 Hangeweza kutenda kwa Wayahudi, kujitangaza Mwenyewe namna hiyo kuwa Myahudi, kwa wote wawili . . . Kuna jamii tatu tu za watu; hizo ni Myahudi, Msamaria na Mmataifa; watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, wale wana watatu wa Nuhu. Hamna lingine. Kwa hivyo kwa Ha- . . . kwa Hamu na kwa watu wa Yafethi, ama, watu wa Shemu, hasa, Yeye tayari amejitangaza Mwenyewe na kuwaachia Mataifa wakati huu, na moja kwa moja katika kumalizika kwake, wakati Sputniki iko angani na maandiko ya mkono yako kwenye ukuta, nayo mataifa yakitetemeka, Huyu hapa miongoni mwetu, akipigwa picha Yake.

97 Ulimwengu wa kisayansi umesimama umeduwaa juu yake. "Hakuna anayeweza kuja," Yeye alisema, "asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Yesu hakufa ili kuuokoa ulimwengu wote, alitaka kuuokoa, lakini alikufa ili kuwaokoa wale ambao Mungu, kwa kujua tangu zamani, alijua wangeokoka. Si watu wote watakaomjia.

98 Mungu humchukua mtu Wake bali kamwe si Roho Wake. Ibilisi humchukua kafiri wake lakini kamwe si roho, inabakia, ndani ya wengine. Nazo hizo roho mbili zinapigana hivi sasa. Naye ni yeye yule jana, leo na hata milele.

99 Nukuu moja zaidi ikiwa mtalipa nafasi kwa dakika moja. Ili ninyi watu . . . Ni usiku mmoja tu, wala hamtapata, ninyi nyote, nafasi ya kusimama katika mstari wa maombi. Sasa, sikilizeni kwa makini ninapofunga.

100 Nimewasomea, na kuwanukulia, ninyi, kutoka katika Neno la Milele la Mungu. Naye Yesu alisema . . . Ni wangapi wanaojua kwamba Yesu alidai kuwa si mponyaji? Mnamaanisha hamwamini hilo? Biblia ilisema, Yesu alisema, Mwenyewe, "Si Mimi nizitendaye kazi hizo; ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzitenda hizo kazi."

101 Yohana Mtakatifu 5:19, alipitia mahali pakubwa mno ambapo palikuwa na vilema wengi na vipofu mara kumi zaidi ya hao, watu wanaoteseka, wanaoketi katika jengo hili usiku wa leo, kwenye lango zuri la kidimbwi. Viwete, vilema, vipofu, waliopooza, Naye huyu hapa anakuja kupitia kwenye ule umati, akitazama huku na huku, mpaka akampata mtu amelala juu ya godoro. Naye akasema, "Wataka kuwa mzima?" Kwa nini hakumwambia, kilema au kipofu?

102 Na yeye akasema, "Sina mtu wa kunitia majini, Bwana, ninapokuja . . ." Angeweza kutembea. Alikuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane; haungemwua; ulikuwa umedumaa. Akasema, "Ninapokaribia majini, mtu mwingine hushuka mbele yangu."

Alisema, "Jitwike godoro lako uende." Huyo akaenda. Wao . . .

Ndipo marabi na makuhani wakamchukua. Kwa hiyo Yesu akaletewa swali. Akasema, "Amin, amin, nawaambia . . . "

Kwa maneno mengine, "Kwa nini usiwaponye wengine wote? Kwa nini usifanye *hivi*? Kwa nini ulifanya hivi siku ya Sabato?"

103 Akasema, "Amin, amin . . . " (Hiyo ni, "Kabisa, kabisa.") " . . . nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda."

104 Baba alimwonyesha mtu huyo alikuwa pale, na katika hali hiyo; jambo lile lile alilomfanyia, yule mwanamke kisimani; wakati uo huo alifanya huko Filipo; huko nyuma. Huyo alikuwa ni Mungu akifanya kazi kupitia Mwanawe. Sasa, usiku wa leo, Mungu yuko ulimwenguni kote katika Kanisa Lake lote kama Mzabibu, nasi ni matawi.

105 Sasa, kulikuwa na mwanamke wakati mmoja ambaye hangeweza kumfikia. Naye akasema moyoni mwake, "Kama nikiweza kugusa vazi la Mtu huyo, nitapata afya."

106 Naye akajipenyeza katikati ya umati, kupitia kwa kuhani wake, na mpaka akafika pale alipokuwa. Na huku kila mtu anampigapiga mgongoni, "Rabi, tuna furaha kuwa na Wewe hapa." Alikuwa akienda Zake kumfufua binti ya Yairo. Ndipo maskini mwanamke huyu akaligusa tu vazi Lake. Sasa, kama umewahi kuona vazi la Kipalestina, linapwaya, nalo lina vazi la ndani. Unaona? Asingeweza kuuhisi huo, kimwili. Aligusa vazi Lake, naye akaenda na kuketi chini, ama akasimama, popote pale, huko nje kwenye kusanyiko. Yesu akasimama na kusema, "Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?"

Naye Petro, akilitazama kama vile mtu angelitazama siku hizi, akamkemea na kusema, "Mbona, unasema ni nani aliyekugusa? Kila mtu anakugusa."

107 Akasema, "Lakini nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka." Mtu fulani aligusa kwa mguso tofauti, vinginevyo. Huo ndio mguso tunaozungumzia, sio dhana ya kiakili, lakini kitu kinachotoka *hapa* ambacho hugusa kweli kweli.

108 Loo, hakika, sisi, "Nilimgusa; niliweka jina langu kwenye kitabu cha kanisa; nilijiunga na kanisa; nilibatizwa; mimi . . . " Huo ni mguso kweli; huo sio mguso ambao Yeye huhisi.

109 "Ni nani aliyenigusa?" Hakuna mtu aliyesema chochote. Naye akatazama kwenye kusanyiko mpaka akampata maskini mwanamke, Naye akamwambia yaliyotukia, shida zake za kutokwa na damu, na kusema, "Imani yako imekuokoa."

110 Ndugu, dada, kama kamwe sitakutana nawe tena, mpaka kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo, ambapo matendo yanayotendwa katika mwili yatadhihirishwa, hebu niwaulize swali hili, mnijibu kwa akili timamu: Ikiwa Yeye ni Kuhani

Mkuu leo anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, si ingemlazimu kutenda vile vile alivyotenda wakati huo, kama Yeye ni yeye yule? Sivyo? Kama unaweza kuketi kwenye kusanyiko hilo pamoja na . . .

111 Biblia inasema . . . Ni wahudumu wangapi hapa wanaojua hilo? Kwamba Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania kilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa ambaye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Ninyi wahudumu inueni mkono wenu. Mnaona? Makasisi; mchungaji wenu anajua hilo. Yeye ni nini? Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

112 Basi kama Yeye anadumu yeye yule jana, leo, na hata milele, angejibuje? Kama alivyofanya jana. Wewe mguse usiku wa leo, useme, "Bwana Mungu, sitakuwa katika mstari huo wa maombi; sina kadi ya maombi, kwa hiyo sitaitwa kule juu; lakini Ee Mungu, nijalie nikuguse Wewe." Uone kile anachofanya. Uone kama Yeye hatendi kazi . . . Kama wewe ni sehemu ya Mzabibu wewe mwenyewe, na Roho Wake hapa, Yeye atajibu moja kwa moja, akitumia karama kudhihirisha na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni yule yule aliyewahi kuwa, haijalishi uko wapi. Amini tu Neno la Mungu usiku wa leo na uliamini kwa moyo wako wote naye Mungu atalidhihirisha. Ikiwa atafanya hivyo mbele zenu, sisemi kwamba atafanya, kama atafanya hivyo, ninatumaini ya kwamba mtamwamini na kumkubali.

113 Pia kumbukeni sasa, tunapofunga. Huu ndio mwisho wa wakati wa Mataifa. Haijawahi kutokea katika historia, mpaka sasa, huu ndio wakati wa mwisho. Tumekuwa na Bw. Billy Graham, Roho mkuu kama Yohana Mbatizaji aliyetoka bila kufanya miujiza.

114 Ni wahudumu wangapi hapa wanaojua kwamba historia, historia ya kanisa, na unabii unajirudia angalau mara moja au mbili? Kweli. Mnaamini. Angalieni Mathayo 3: "Kutoka Misri namwita Mwanangu." Rejelea hiyo uone kama hakuwa Yakobo. Huyo alikuwa mwanawe, pia. Mnaona? Historia hujirudia.

115 Basi kulitokea Roho mkuu, katika tu Kuja Kwake mara ya kwanza. Kulitokea Roho mkuu kabla ya kuangamizwa kwa Wayahudi, kwa mfano wa Yohana Mbatizaji, ambaye hakufanya miujiza hata kidogo bali alikuwa mhubiri hodari. Baada yake akaja Roho ambaye hakuwa mhubiri mwenye nguvu, lakini ishara tu na maajabu yakaanza kutokea kila mahali. Mwishoni tu mwa huo wakati. Huu ndio mwisho wa wakati wa Mataifa. Na tuombe.

116 Bwana Mungu, ni vigumu sana, Bwana, kujaribu kunena yote yaliyo moyoni mwako katika ujumbe mmoja mdogo uliokatikakatika, tukijua kwamba kunaweza kuwa na watu hapa ambao wataninii . . . hatutaonana tena uso kwa uso, mpaka tutakapokutana Siku hiyo huko ng'ambo miguuni Pako.

117 Ee Mungu, na tutende usiku wa leo kama Wakristo halisi, kama wana na binti halisi wa Mungu. Utupe imani ya kuamini Neno Lako na kusimama. Wakati tunaposoma katika siku za zamani, wakati wanaume na wanawake ambao walikuwa waoga, waliporudi nyuma, na hata wale kama Nikodemo, walioteleza huku na huku. Lakini, loo, jinsi tunavyovutiwa na yule aliyetoka moja kwa moja na kuchukua msimamo wao.

118 Mungu, ninaomba usiku wa leo, ya kwamba utafanya hivyo kwa kila mmoja humu ndani, wape ba—baraka kubwa sana ya kutenda kazi kwa Roho, ili kila mtu humu ndani wachukue nafasi yao kama waaminio halisi. Tujalie, Bwana.

119 Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Nasi tunafundishwa katika Maandiko kwamba wakati, siku moja, siku ya kwanza baada ya Wewe kufufuka katika wafu, kwenye asubuhi hiyo ya kwanza ya Pasaka, kulikuwako na watu wawili waitwao… jina la mmoja wao, na hilo, hatuwezi kujua; na huyo mwingine alikuwa Kleopa; nao walikuwa wakienda zao kwenye mji mwingine mdogo uitwao Emau. Basi walipokuwa wakienda zao wakizungumza juu ya Maandiko, na juu Yako, ulijitokeza moja kwa moja kutoka kichakani na kutembea pamoja nao siku nzima. Wala hawakutambua Wewe ulikuwa ni Nani.

120 Na, Baba, nina hakika, usiku wa leo, ya kwamba watu hawa wanaweza kuelewa ya kwamba tunajaribu tu kunena Neno la Mungu, mambo ambayo ameahidi. Nawe ulinena nao siku hiyo juu ya Neno. Nao walipofika kwenye maskini nyumba ya wageni, jioni, walikualika uingie. Nawe ulipoingia ndani na kuufunga mlango, ulifanya kitu kama vile tu ulivyokuwa ukifanya kabla ya kusulubiwa. Na kwa njia hiyo wakajua kwamba umefufuka katika wafu. Upesi, wakakimbilia kwa ndugu zao na kusema, "Kwa kweli Bwana Yesu amefufuka katika wafu. Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Mungu, jalia huo uwe ushuhuda wa watu hawa, usiku wa leo, wanaorudi chini mjini, mahali mbalimbali.

121 Njoo, Yesu, na useme na mioyo yetu na ufanye jambo fulani hapa usiku wa leo; ili wanaume na wanawake, wavulana na wasichana wapate kujua, kwamba baada ya kulisoma katika Biblia, jinsi ulivyotenda kule nyuma katika siku hiyo, na kudai Wewe ni yeye yule leo, tenda katika kanisa Lako usiku wa leo, vivyo hivyo, Baba; ili watu waseme, wakienda zao nyumbani usiku wa leo, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliposema nasi njiani?" Tujalie, Bwana, na sifa zitakuwa Zako, katika Jina la Mwanao, Yesu. Amina.

122 Sasa, huu ndio wakati ambao nitauliza, kama utaninii… itakubidi uondoke katika dakika kumi na tano hadi ishirini zijazo, unapaswa kuondoka sasa. Sitaki mizunguko wakati Roho Mtakatifu, kama akija kutenda, mnaona, Yeye…Inawapasa kuwa na kicho kikamilifu, na uangalie, na usikilize. Kwa

hivyo kama huna budi kuondoka, ningefanya hivyo sasa, ili usiukatishe mkutano. Wao huniondoa mkutanoni kunapokuwa na kukatizwa.

123 Na sasa, kama wewe ni mkosoaji, ama asiyeamini, nisingekaa katika mkutano wa aina hii wakati huu unapoendelea, kwa sababu msomaji yeyote wa Biblia anajua, kwamba pepo wachafu hutoka kwa mtu mmoja wakaingia kwa mwingine. Tunakubaliana na hilo. Kwa hivyo sio kuigiza kanisa.

124 Hapa siku chache zilizopita usiku, mngewasikia Anania na Safira fulani, kama isingalikuwa ni rehema za Mungu. Na ni mara ngapi nyinyi watu mmesikia, kama ibada zenye kicho, jinsi mambo yanavyotendeka hivyo wakati wa mkutano? Kwa hiyo iweni na uchaji kabisa, watulivu, ketini, mkipendana, iweni katika maombi.

125 Sasa, naamini . . . Je, ulisema ilikuwa . . .? Kadi zipi za maombi? Mia moja, ulizisambaza? Zipi? Y, mia moja. Vema, hatuwezi kuwaleta wote mara moja, ningeomba, basi, kadi za maombi Y, moja, mbili, tatu, nne, tano. Acha waje kwanza. Vipi . . .? Je, tunaweza kuwaleta kupitia huku, bwana? Ni nani aliye na kadi ya maombi Y, namba moja? Unaweza kuinua mkono wako? Kama unaweza kusimama; sasa, ikiwa huwezi, mtu fulani atakubeba. Kadi ya maombi . . . Igeuze; ni kadi ndogo mraba yenye namba na herufi. Unayo hiyo, mama? Y, namba moja? Y, kama y-o-u? Y, namba moja, inua mkono wako, popote ulipo. Katikati, huyo msichana hapo? Njoo huku, dada.

126 Y, namba mbili, unaweza kuinua mkono wako? Angalia kadi ya jirani yako; anaweza kuwa kiziwi, bubu, hawezi hata kuongea wala kusikia. Unayo namba mbili? Njoo papa hapa, mama. Namba tatu? Kadi ya maombi namba tatu, unaweza kuinua mkono wako tafadhali? Je, unaweza kuja hapa, mama? Namba nne? Inueni tu mikono yenu haraka ili tuweze kuona tulipo . . . Namba nne? Kadi ya maombi . . . Juu sana kwenye roshani? Vema, namba nne, shuka moja kwa moja, kadi ya maombi namba nne. Namba tano?

Sasa, hao wavulana hushuka huku, wanazichanganya kadi hizi zote, na kuwasambazia tu, na hivyo—hivyo ndivyo tulivyo nazo.

127 Namba tano? Je, kuna mtu yeyote aliye na kadi ya tano ya maombi? Tikisa mkono wako, au punga mkono wako, tupate kujua. Vema. Sita? Kadi ya maombi sita, inua mkono wako? Vema, mama, hiyo ni sawa. Namba saba, namba saba? Nane?

128 Sasa angalieni sasa, ili kwamba hakuna mtu . . . mtu fulani huenda akawa ni kiwete (na wanapofanya hivyo, inatubidi kuwabeba, mnaona), kama ni mtu aliye kiziwi na bubu.

Nane, tisa, kumi? Tisa, kumi? Vema. Kumi na moja, kumi na mbili? Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano? Naam, bwana? Vema, hebu kidogo.

129 Vema. Sasa, wakati wakija, hebu nizungumze nanyi tena. Njia hii nyingine, mama, tafadhali, papa hapa, njoni huku, tungeni mstari wenu. Vema, wakati wakizungumza-. . .wakati nikizungumza, nao wanajipanga, kwa muda kidogo tu.

130 Sasa, nitaomba kwamba kila mtu awe na uchaji na utulivu kadiri mwezavyo. Sasa, ninajua ya kwamba mara nyingi Mungu huwabariki watu, nao wanapiga mayowe; hiyo ni sawa kabisa. Mimi ni mtu wa Kusini, nimezoea hilo. Mnaona? Hilo halisumbui.

131 Lakini sasa msipige picha zozote, msiache nuru imulike, ama chochote kile; iweni tu na kicho. Maana Roho Mtakatifu ni Nuru. Ni wangapi wanaojua jambo hilo, wanaojua kwa Maandiko kuwa ni Nuru?

132 Sasa, ni wangapi humu ndani ambao hawana kadi ya maombi, popote pale jengoni, haidhuru uko wapi, huna kadi ya maombi, hata hivyo unataka Yesu akuponye? Inua mkono wako. Useme, "Nataka Yesu aniponye," inua mkono wako tafadhali, ili nipate dhana ya jumla. Vema, hilo ni sawa kabisa. Vema, sasa uwe na kicho sana.

133 Sasa, jambo. . .Usipopanda hapa jukwaani, mtazame tu Kristo na kusema, "Bwana Yesu, kama mtu huyu ameniambia kweli, ambayo naamini ameniambia, basi Wewe nena nami." Nami si ninii. . .Usijaribu kujipenyeza sasa; tulia tu, useme, "Bwana, naungama dhambi zangu; yote niliyokosea, nisamehe hayo. Na uniponye, Mungu mpendwa. Lijalie." Ona jinsi Mungu alivyo na rehema.

134 Na sasa, hiyo. . .Sasa, kila mtu hapa ndani, nijuavyo mimi, hatufahamiani kabisa; ili watu ambao wanaweza kuwa wameketi karibu. Watu pekee ninaowajua katika jengo hili ni Bw. Sweet, Dk. Vayle, na mvulana wangu, kil-. . .Nafikiri ndiye yule anayesimama kule nyuma gizani; sina uhakika. Hao ndio pekee ninaowajua.

Wangapi hapa hatufahamiani? Inueni mikono yenu. Siwajui ninyi; sijui lolote kuhusu. . .katika mstari wa maombi kwa njia iyo hiyo? Sasa, vema.

135 Sasa, tutaona ama kama Neno ni kweli au si kweli; mimi kusema kweli, au sio kweli. Mungu hushughulika tu na ukweli, tunajua hilo. Mtu anaweza kukiri chochote anachotaka, lakini kama Mungu hakiungi mkono, na kusema ni kweli, basi ni makosa. Ninadai ya kwamba Neno Lake ni lile lile, Naye anadumu yeye yule, wala hawezi kuwa kitu kingine ila Mungu yeye yule, naye hana budi kutenda vile vile ambavyo Yeye amekuwa akitenda daima.

136 Na kama atafanya jambo hilo hapa jukwaani, nje kupitia kwa wasikilizaji, na kujitangaza Mwenyewe Yesu aliyefufuka, ikiwa nyote mtampenda na kumwamini, semeni,

"Amina," Kwake. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu awabariki.

137 Sasa, baada ya kunena, nina hakika mnatambua ya kwamba mahali ninaposimama, niko mahali pa namna gani. Naye Mungu, ambaye ni Hakimu wangu mkuu, anajua, mwanamke huyu, ama yeyote kati yenu ninyi watu ambao sijawaita, katika mstari wa maombi ama chochote kile, siwajui. Basi Kitu fulani hakina budi kutenda sasa, la sivyo Maandiko si sahihi, kwa sababu nimesoma mambo haya kutoka katika Maandiko, ambayo ni ahadi ya Mungu. Je, mnaamini hiyo ni kweli? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

138 Ni ahadi ya Mungu. Aliahidi angefanya hivyo. Si lazima afanye hivyo, bali hana budi kulifanya kwa njia ya kusema ya kwamba Yeye aliahidi angelifanya, hivyo ndivyo afanyavyo. Anafanya-. . . Ha—haikumbidi kuponya alipokuwa hapa duniani, bali alifanya hivyo ili jambo hilo litimie.

139 Hivyo ndivyo Yeye anavyofanya leo: kuumalizia wakati wa Mataifa; awarudie Wayahudi; Kanisa liende Nyumbani; uharibifu uje kwa ulimwengu, hayo hapo maangamizi yako; imekwisha. Unaona?

140 Nanyi mnaona, jambo pekee ambalo lingehitaji ili kutukia usiku wa leo, ni vinywaji vichache vya vodka. Tayari yameelekezwa. Mnaona? Hakuna unachoweza kufanya juu yake. Bila shaka tuna kitu kile kile cha kurushia huko tena. Inafanya nini? Kuurusha ulimwengu kutoka kwenye mzingo wake, kama tu Biblia inavyosema, naye huyo anaenda.

141 Mnakumbuka yale Yesu aliyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu"? Kuna mtu aliyewahi kusoma hilo? aseme, "Amina." Ilikuwa ni nini? Kabla ya Lutu kuangamizwa, au, Sodoma kuangamizwa, kuna Malaika aliyekuja kwa Mteule, ambaye alikuwa ni Ibrahimu, sivyo?

142 Naye alipofanya hivyo, aliketi chini, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Naye akamwambia Sara, ama, akamwambia Ibrahimu, "Kuhusu nitakurudia, wakati huu huu mwakani. Sara atampata mtoto huyu ambaye umemngoja, kwa miaka ishirini na mitano."

143 Naye Sara, huko nyuma kwenye hema, nyuma ya hema, nyuma ya huyo Malaika, akatabasamu. Naye huyo Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Ni wangapi humu ndani waliowahi kusoma jambo hilo? "Kwa nini Sara akacheka?" Alikuwa nini? Mpiga ramli, telepathia? Kumbuka, Malaika huyo alikuwa na ujumbe wa mwisho ambao Sodoma ilipokea kabla haijaangamizwa.

"Kama ilivyokuwa," alisema Yesu, "katika siku za Sodoma."

144 Sasa, kumbuka, ni Uwepo wa Malaika wa Mungu, Roho Mtakatifu, aliye hapa leo pamoja na kila kitu cha kisayansi na ishara na maajabu ambayo amewahi kuahidi, kuwatimizia ninyi watu. Ninyi Wakristo mnapaswa kuwa na furaha.

145 Sasa, namgeukia yule mwanamke. Sasa, mama, mimi na wewe tukiwa hatufahamiani, na hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Ninakushinda umri kwa miaka kadhaa, na hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini hili, kwa wasikilizaji, unaposoma Yohana Mtakatifu 4, angalia jambo hili, jambo lile lile hasa: Bwana wetu alikutana na mwanamke ambaye hakuwa amemwona maishani Mwake, na kama vile katika mandhari ndogo, kama nilivyosema muda mfupi uliopita, namna *hii*. Sasa, huyu hapa, Naye akapata mahali shida yake ilipokuwa, na akamwambia shida yake ilikuwa ni nini. Naye akasema, "Huyu ndiye Masihi."

146 Sasa, mimi sikufahamu, dada yangu, sijui kama wewe ni Mkristo, kama wewe ni kafiri, jinsi maisha yako yalivyo, jinsi yamekuwa; si—sijui; sina njia ya kujua; sijui lolote kukuhusu. Lakini kama kitu fulani, nguvu za kimbinguni za Mungu, kupitia Malaika huyu, hapa, zitakuja na . . .

147 Kama nikikuambia, "Mama, wewe ni mgonjwa; utapona; endelea"; ungekuwa na neno langu tu; hilo ndilo tu ungejua. Ambapo, hiyo ingeweza kuwa sawa.

148 Lakini kama Yeye akija na kukwambia jambo fulani maishani mwako, utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Wewe utakuwa mwamuzi wa hilo. Basi kama anajua yale yamekuwako, bila ya shaka Yeye angejua . . . Kama angeweza kukwambia kilichokuwa, ungekuwa na ujasiri wa kujua ya kwamba kile anachosema kitakuwa, kitakuwa. Sawa? Kwa sababu ingekuwa ni Mungu; ungeamini ingekuwa ni Yeye? Yesu? Ungeamini hivyo? Bwana alijalie, ndilo ombi langu.

149 Sasa, kusanyiko linaposubiri kwa kicho, nanyi ni ku—kundi la watu wenye uchaji, hii ndiyo ile saa. Sasa, kama wewe . . . ikiwa huyu mwanamke, kwa uaminifu moyoni mwake, anajua ya kwamba jambo fulani linaendelea. Hangeweza kujisikia jinsi anavyojisikia sasa, akiwa amesimama mbele ya mwanaume. Ningekuwa mwanaume kama baba yako, ndugu, mume. Lakini kuna jambo ambalo ndiyo kwanza lianze kutokea, hisia ya unyenyekevu, tamu, inayokujia. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, hakika. Unaona? Malaika huyu, unaona picha Yake, kati yangu na wewe, ni nuru halisi tu.

150 Huyu mwanamke hasimami hapa kwa nafsi yake mwenyewe, amesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine; hakuna kitu kibaya na huyu mwanamke, nje ya wasiwasi. Yeye ni mtu mwenye wasiwasi ambaye ana wasiwasi juu ya mambo, huku akihofia sana mambo kabla hajayafikia. Lakini uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli.

151 Ikiwa Bwana Mungu atanifunulia kile kimekuleta hapa, je, utamwamini Yeye kuwa ndiye Masihi, na utaenda kuwaambia wengine kwamba Masihi bado yu hai? Utawaambia? Unaamini hilo jicho dogo litanyoka, la huyo mtoto? Jicho kombo, lenye makengeza, unaamini ya kwamba Yeye ata—ataliponya? Utaamini? Una kitu kingine moyoni mwako pia, sivyo, mbali na mtoto huyo? Ni mama yako, anakufa; ana kansa. Hiyo ni kweli. Nawe unahofu kuhusu wokovu wake kwa sababu yeye ni Mkatoliki. Hiyo ni kweli. Usijali, kuwa na imani. Mpelekee leso hiyo; usiwe na shaka, utapata ulichoomba. Mungu akubariki, nenda, na uamini sasa na kupokea. Mungu akubariki, dada.

Unaamini? Sasa, muulize mwanamke huyo, anaweza . . . Ungemjua. Iweni na kicho kweli sasa, tafadhali.

152 Je, mnatambua, ndugu wahudumu, kwamba Kristo ambaye ninyi na mimi tumemtetea (mimi kama mhubiri wa Kibaptisti kwa miaka ishirini na saba katika huduma), huo ndio Uwepo Wake hapa sasa kuthibitisha kabisa? Ni wangapi wanaojua hivyo ndivyo tu alivyofanya alipokuwa hapa duniani? Hebu tuone mkiinua mikono yenu, ninyi watu popote pale. Biblia, hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyosema.

153 Basi, kama hii ndiyo ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, kama Ndiyo iliyokuwa hapa duniani na kusema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nitakapoondoka; nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu": Mzabibu uo huo ungezaa matunda yale yale, sivyo? Vema, Hii hapa, ikifanya jambo lile lile. Usikose kuamini. Kila mmoja wenu, sasa hivi, anapaswa kuamini.

154 Hatufahamiani, nadhani, mama? Mara ya kwanza kukutana maishani. Ikiwa ningeweza kukusaidia na nikatae, ningekuwa mtu katili. Lakini ni—nina mama mzee nyumbani usiku wa leo, nami na—nampenda; nami niliacha familia, mama, na wote, kuja hapa kujaribu kusaidia, kufanya maisha yawe ya kupendeza zaidi kidogo kwa watu, na kufanya yote niwezayo kama mtumishi Wake. Kama Bwana Mungu angeniambia kilichokuleta hapa, ungeniamini? Na kuamini ya kwamba ni Yeye anayefanya jambo hilo? Je, kusanyiko lingeamini? Mama huyo, anaugua ugonjwa wa wasiwasi, ana ugonjwa wa moyo, na ana mishipa iliyovimba. Hiyo ni kweli kabisa. Unaamini sasa?

155 Unasema, "Bw. Branham, ulibahatisha hilo." Sikubahatisha. Mungu anajua hilo. Hebu tuzungumze naye zaidi kidogo. Je, ungelishuku? Bwana na alijalie.

156 Naam, kuna mtu mwingine hapa ambaye ana haja pia, huyo ni mume wako. Anakufa, hana budi kufa mara moja ikiwa Mungu hatamsaidia. Ana leukemia; hiyo ni kansa kwenye mkondo wa damu. Hiyo ni kweli; hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Harford. Jina lako ni Rose na lake ni Robert. Hiyo ni kweli. Nenda zako, mwamini Mungu upate kuishi, mama. Mwamini

Mungu, Yesu Kristo, aliyepo. Unajua huyo ni Yeye hapa? Vema, mkubali Yeye sasa kama Mponyaji wenu kwenu nyote wawili, kisha uende zako na Bwana Mungu akubariki sana, dada yangu.

Unaamini? Kuwa na imani. Usiwe na shaka. Sasa, amini tu, kwenye kusanyiko.

157 Hatufahamiani, nadhani, mama. Mara ya kwanza tumekutana. Ni. . . Sasa, wewe. . . kama wewe ni mgonjwa ni—nisingeweza kufanya lolote kuhusu hilo kwa sababu mimi ni mwanadamu tu. Lakini Mungu anaweza kufanya jambo fulani kulihusu. Sasa, kama Yesu alikuwa amesimama hapa akiwa amevaa suti hii, ungesema, "Bwana Yesu, niponye."

158 Angesema, "Tayari nimefanya hivyo." Unaona, uponyaji ni kitu kama wokovu; umepita. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Tayari imekamilika katika upatanisho. Tunaamini tu.

159 Hakuna chochote ningeweza kufanya. Unaona? Ingekuwa vile angeweza. . . Tayari amefanya. Ni imani yako kuninii. . . Sasa, huenda akakwambia jambo fulani kukufanya uamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi halafu kwa jambo hilo ungeamini ya kwamba upatanisho ulikuwa sahihi. Na haya ndiyo aliyoahidi angefanya; kutenda kazi moja kwa moja. Wewe ni mwaminio, mwaminio Mkristo. Ungeweza kuwa kafiri, mkosoaji, lakini sivyo.

160 Jambo lile lile kwa mwanamke huyu aliyeketi humu. . . aliyeketi pale chini kabisa, mwishoni mwa kiti. Nguvu hizo nyeusi, za pepo. Mwanamke huyu anaugua ugonjwa mbaya sana; ni kweli kabisa. Wasiwasi na sikuzote unahofu. Una ugonjwa wa moyo; na hiyo ni kweli. Nawe una wasiwasi, na una hali ya kutisha. Halafu unaogopa pia; umekuwa na jambo lililokupata, hapa wakati fulani uliopita, ulikuwa na fundo lililotolewa, ama uvimbe, kutoka kichwani, nao unarudi tena.

161 Maskini mama huyo aliyeketi pale anaugua wasiwasi wa akili. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli msichana. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya pia? Naam, unaamini? Unaamini? Inua mkono wako kama unaamini. Nyote wawili mmeponywa. Nendeni zenu mkishangilia. Yesu Kristo anawaponya. Usiuogope tena; yote yamekwisha sasa, nenda zako nyumbani. Anadanganya tu, huyo pepo alikuwa anadanganya, lakini ametoka ndani yako sasa. Nenda zako tu ukiamini, ukiwa na imani.

Mnampenda? Yeye ndiye Alfa na Omega mkuu.

162 Sasa, jambo lingine lilifanyika wakati huo tu. Iweni na kicho kabisa, tafadhalini. Kuna mama ameketi karibu mwishoni pale huku ameinua mikono yake *hivi*. Anaugua ugonjwa wa jicho; ana shida ya macho yake. Naye ana ugonjwa wa moyo pia. Ulikuwa unaomba, sivyo, mama? Mama huyo aliyeketi papo hapo karibu na mtu huyo ambaye amegeuka na kumwangalia mkewe. Inua

mkono wako, mama. Hiyo ni kweli. Sikujui, sivyo, mama? Hatufahamiani. Unaamini sasa kwamba utakuwa mzima? Vema, nenda nyumbani, sahau hilo. Mpe Mungu sifa. Imani yako inakuponya.

Ninawapa changamoto muamini. Angalieni, iweni na kicho sasa. Msizunguke-zunguke.

163 Mama, hatufahamiani? Una hofu, huzuni. Loo, ni kuhusu mvulana huyu. Hiyo ndiyo sababu ya kumleta hapa; ndio kwanza umlete hapa. Hiyo ni kweli. Ikiwa Bwana Mungu wetu atanifunulia jinsi unavyohangaika sana juu ya mvulana huyu, utakubali na kuamini yanatoka kwa Bwana Mungu wetu? Mvulana huyo yuko tayari kufanyiwa upasuaji, naye daktari anasema kwamba kuna uvimbe kwenye moyo wake ambao lazima utolewe. Hiyo ni kweli, sivyo? Nawe una wasiwasi juu yake. Ikiwa Mungu yuko hapa na anajua kuhusu mtoto huyo, hivi Yeye si anamjali? Je, utamkubali kama mtoto wako kuishi, na utamlea kwa utukufu wa Mungu? Tuombe.

164 Mungu mpendwa, ninadai uhai wa mtoto huyu, kupitia kwa Yesu Kristo, na awe mzima. Mama yake na abarikiwe. Na jamii ibarikiwe. Kwa kuwa tunaomba haya katika Jina lililobarikiwa la Bwana Yesu. Amina.

Usiwe na wasiwasi sasa, kuwa na imani mwanangu jamani; utakuwa mzima.

165 Njoo mama. Sikujui. Bwana Mungu anakujua. Ikiwa atanifunulia shida yako ni nini, je, utamkubali Yeye kama Mponyaji wako? Iweni na kicho kabisa. Unaugua ugonjwa wa tumbo na ugonjwa wa ini; ini linausababisha hasa, linaimiminia nyongo tumboni na kulitupa kwenye mshtuko. Hiyo ni kweli. Nami ninakuona ukifanya jambo fulani kujaribu ku- . . . Loo, huna ladha yoyote; umepoteza hisia zako za ladha. Huna ladha au harufu yoyote, hata moja. Hiyo ni kweli. Unaamini unayo sasa? Songa mbele, hiyo ni kweli. Mungu akubariki.

166 Kuna wengi humu jengoni wanaoteseka na kitu kile kile ulicho nacho. Lakini Mungu anaishi moyoni. Unaamini anaweza kuponya ugonjwa wa moyo na kukupa afya? Unaamini? Tuombe.

167 Bwana Mungu, mhurumie mwanamke huyu kwa ajili ya utukufu Wako ninapoomba, katika Jina la Yesu. Amina. Usiogope. Nenda ukiamini sasa, kwa moyo wako wote, usiwe na shaka.

Ulikuwa na jambo lile lile, kwa hiyo endelea tu kusonga mbele, ukimwamini Mungu.

168 Je, mnaamini, nje kwenye kusanyiko? Tafadhalini, sasa, iweni tu na kicho mwezavyo. Kicho, tafadhalini, kila mtu.

169 Unaamini Mungu anaweza kukuponya hiyo yabisi kavu, unayeketi hapo, bwana, akupe afya? Huyo mzee muungwana

anayeketi hapo amevaa hilo koti dogo, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini?

170 Aisee, wewe u—uliyemgusa basi. Wewe ni mtu mzuri. Unaamini kuwa tatizo lako la mguu litakuwa sawa? Jina lako ni Bw. Young, sasa, nawe unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema, hilo lilikuwa ni jambo la kutelezea tu ili niweze kukukamata. Naona ni wewe ulikuwa ukiamini kwanza kabisa.

Mnaamini?

171 Huyu mama, anayeketi hapa chini, yule mama wa pili, kwa namna fulani ni mnene, anaugua shinikizo kuu la damu, anayeniangalia moja kwa moja, katika safu ya kwanza hapo, unaamini Bwana Mungu anakuponya, dada? Unaamini? Je, unaweza kuukubali kama uponyaji wako? Inua mkono wako kama unaukubali. Hilo ni sawa. Inua leso yako juu sana, usione haya; kwa imani namna hiyo, ungeweza kumgusa Mungu. Kuwa na imani.

172 Huko chini kabisa mwishoni mwa safu, aliyeketi pale kati ya wanaume wawili, yule mama mwenye shinikizo kuu la damu, safu ya pili nyuma, mwishoni, je, unaamini kwamba Yesu Kristo atakuponya shinikizo lako kuu la damu? Ilitokea kwamba, niliona mchirizi ukimwacha mama huyu na kwenda kwako; hiyo ndiyo sababu nilijua ya kwamba unaweza kuponywa, ukitaka kuukubali.

173 Ninaipa imani yako changamoto. Hapa kuna mtu mpendwa ameketi hapa, papa hapa nyuma, ameketi pale, amevaa kofia ndogo nyeusi, ana matatizo ya kichwa chake, anayaombea. Hiyo ni kweli, sivyo, dada? Papa hapa, maskini mama huyo aliyevaa kofia nyeusi na miwani, unaumwa na kichwa chako; lakini huumwi sasa, sivyo? Uliponywa papo hapo.

174 Mama aliyeketi karibu nawe anaonekana kama... Unaamini, mama? Ninataka tu kuwasiliana na roho yako. Weka mkono wako juu ya huyo mama aliye karibu nawe hapo. Mama huyo ambaye ndio kwanza aponywe, weka mkono wako juu ya mama huyo mwingine. Naam. Unaamini Bwana Mungu atakuponya, mama? Una matatizo, mambo mengi yanayokusumbua, kama vile kisukari, kwanza, ugonjwa wa moyo, ni mwingine. Hiyo ni kweli. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, nenda zako nyumbani, amini kwamba yamekwisha, yataondoka.

175 Maambukizi hayo...maskini mama huyo aliyeketi chini yako hapo, unaamini ya kwamba utaponywa ugonjwa huo wa kuambukiza, mama? Unaamini, maskini wewe mama hapo? Bibi Hunter kutoka Caribou, simama. Sikujui, sivyo, mama? Sijawahi kukuona, sivyo? Najua sauti yangu inarudisha mwangwi. Hatufahamiani, kama hatufahamiani, inua mkono wako. Hiyo

ni kweli. Je, mambo hayo ni kweli, ambayo yamesemwa? Vema, rudi nyumbani ukapone; Yesu Kristo akuponya.

Unawazia nini kuhusu hilo, mama? Unaamini ya kwamba umeponywa sasa? Nenda zako ukishangilia; hiyo ndiyo njia ya kufanya hivyo. Amina.

176 Ugonjwa wa wasiwasi, umesababisha moyo wako kupepesuka, na kadhalika, hiyo ni kweli, kweli, ambayo ilikuwa kuvimbiwa. Kuna kwingi sana humu ndani. Wangapi wanateseka . . .? Hebu niwaonyeshe. Ni wangapi humu ndani wanaougua ugonjwa wa wasiwasi? Inueni mikono yenu kwa dakika moja. Unaona, utaliitaje hilo? Unaona, ni kila mahali. Ninyi nyote wenye ugonjwa wa wasiwasi simameni kwa miguu yenu. Simameni kwa miguu yenu kama mnataka kumpokea Kristo sasa hivi. Sikilizeni; simameni papa hapa kwa dakika moja, tafadhali.

177 Njoo hapa mama, ama, mwanamume huyo. Njoo hapa, bwana, sikujui, sivyo? Hatufahamiani? Sasa, ili watu wajue sio kuyasoma mawazo yako, weka mkono wako juu ya wangu. Ikiwa Mungu atanifunulia kwa njia hii shida yako ni nini, utaikubali? Utakubali? Ugonjwa wa tumbo, inua mkono wako kama hiyo ni kweli.

178 Kila mtu aliye na tatizo la tumbo simama kwa miguu yako. Kote jengoni simameni kwa miguu yenu, wenye ugonjwa wa tumbo. Simama papa hapa, kwa dakika moja, bwana. Utauona utukufu wa Mungu. Kama unaweza kuamini!

179 Ugonjwa wa mgongo, simama moja kwa moja hapa nyuma. Wote wenye tatizo la mgongo simameni kwa miguu yenu. Sijali ni muda gani umepooza, au umelala chini, simama kwa miguu yako. Unaweza kuona utukufu wa Mungu.

180 Je, mnaamini ya kwamba Uwepo Wake upo hapa? Je, mnaamini kwamba Bwana Yesu Kristo yupo? Kama ndivyo, inueni mikono yenu, kila mtu jengoni. Simameni kwa miguu yenu, kila mmoja wenu basi; simameni, kila mmoja. Sijali kama hukuweza kuamka dakika chache zilizopita, unaweza sasa. Simama. Haya basi.

181 Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, ninadai kwamba Kristo alikufa kwa ajili yako pale Kalvari, ambaye akusamehe dhambi zako na kuponya ugonjwa wako. Uwepo Wake, Yeye aliyeko hapa sasa kudai kwamba amefufuka kutoka kwa wafu, ametangaza kwa uthibitisho usioweza kukosea, kwamba Yeye angali yuko leo na hawezi kufa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

182 Wote wanaoamini hilo, inueni mikono yenu. Biblia ilisema, iliahidi, ya kwamba Yeye angekuwa hapa katika siku hizi kufanya mambo haya. Alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ni wangapi walio waumini? "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Weka mikono yako juu

ya mtu aliye karibu nawe, kama wewe ni mwaminio. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo.

183 Haya basi, katika umoja mkamilifu wa Roho, umoja mkamilifu, huku mikono imewekwa juu yako, umoja mkamilifu pamoja na Roho Mtakatifu, umoja mkamilifu pamoja na nguvu za Mungu, umoja mkamilifu katika Maandiko, basi hayana budi kwisha. Hebu tuinamishe vichwa vyetu huku sote tukitoa maombi kwa Mungu.

184 Bwana Mungu, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Uwepo Wako mkuu, Roho Mtakatifu ambaye yuko hapa sasa kuchukua mamlaka na kutawala kila ugonjwa kutoka kwenye jengo hili.

185 Loo, Shetani, umeshindwa vita, umewadanganya watu kote katika nyakati, lakini saa imewadia, kwa kuwa umefichuliwa. Toka ndani ya watu hawa, maradhi, ninakuamuru kwa Jina la Yesu Kristo, Yule aliyeko hapa kukushinda na amekushinda, liache kusanyiko hili, katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani ya hawa watu.

186 Wote wanaomkubali Mungu kama Mponyaji wako, Kristo kama Mponyaji wenu, inueni mikono yenu Kwake. Amina. Sawa, tupe sauti, *Nitamsifu*. Kila mtu sasa, jifungie tu ndani na hebu tumwabudu Yeye. Vema.

Nitamsifu,

Sote kwa pamoja sasa.

. . . nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwani Damu Yake imeondolea mbali kila . . .

Je, unaweza kuutambua Uwepo Wake? Hebu tuinue mikono yetu tunapoimba.

Nitasifu . . .

Kumbukeni, mwabuduni, tuko katika Uwepo Wake.)

. . . nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo . . . (Ndivyo
hivyo . . . ? . . . )
Mpeni utukufu enyi watu wote . . .

58-0515 Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele

National Guard Armory

Fairfield, Maine Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org